

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE**

**015/2**

**ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**


(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shulen)

**Muda: Saa 2:30**

**Alhamisi, 15 Novemba 2018 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D zenyе jumla ya maswali **kumi na mbili (12)**.
2. Jibu maswali **manne (4)**, swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyohusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



1

Ukurasa wa 1 kati ya 3

CC-18/CSEE

Find more free educational resources at:

<http://maktaba.tetea.org>



## BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIM

### SEHEMU A: QUR'AN

1. "*Tuongoze katika njia iliyonyooka. Njia ya wale uliowaneemeshaa, sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea*". (1:6-7)
  - (a) Kwa nini mwanadamu anahitaji mwongozo kutoka kwa Allah (s.w)? Toa sababu nne.
  - (b) Toa maelezo kuhusu walioneemeshwa, waliokasirikiwa na waliopotea.
2. Andika tafsiri ya Suratul- Bayyinah, kisha chambua mafunzo manne yatokanayo na Sura hii.
3. Madai ya kuhusishwa Mtume (s.a.w) na utunzi wa Qur'an yamewasilishwa kwa sura tofauti kama vile Qur'an ni:
  - (a) Mashairi aliyotunga Muhammad.
  - (b) Zao la njozi zilizovurugika.
  - (c) Kitabu kilichotungwa na Muhammad ili ajiungishe kiuchumi.Toa maelezo mafupi kuhusu madai hayo na kila dai toa hoja moja kuonesha udhaifu wake.

### SEHEMU B: TAWHID

4. Jadili sababu tano zilizosababisha kutohitajika kulekwa Mtume mwingine baada ya Muhammad (s.a.w).
5. "Na walikuwa wakisema: *Tutakapokufa na kuwa udongo na mifupa ndio tutafufuliwa?*" (56:47). Kwa kutumia aya hii;
  - (a) waelimishe wenye shaka ya kufufuliwa. Tumia nukta tatu.
  - (b) eleza taathira ya kuamini siku ya mwisho. Tumia nukta tatu.
6. Kwa kutumia hoja sita, onesha udhaifu wa kubagua elimu katika mtazamo wa dini na dunia.

### SEHEMU C: FIQH

7. Kwa kuzingatia nguzo za matamshi ndani ya swala, eleza mambo nane yanayodhihirisha kuwa lengo la swala halifikiwi na wengi wanaoswali.
8. Chambua maeneo manne ya subira katika Uislamu.
9. "*Wala msikaribie zinaa, hakika hiyo zinaa ni uchafu mkubwa na ni njia mbaya kabisa*" (17:32). Kwa kuzingatia aya hii, bainisha madhara sita ya zinaa katika jamii.

#### **SEHEMU D: TAREKH**

10. Kwa kutumia hoja sita, bainisha vitimbi vyat wanafiki dhidi ya dola ya Kiislamu Madina, wakati wa uongozi wa Mtume (s.a.w).
11. Eleza mafunzo sita wanayopata Waislamu wa leo kutokana na hatua ya Mtume (s.a.w) kulingania Uislamu kwa siri na kwa dhahiri.
12. "Mtume (s.a.w) hakuwa tu kiongozi wa dini bali pia alikuwa ni mwanasiasa mahiri". Jadili kauli hii kwa kutumia hoja sita.